

ZIJUE HATUA ZA KUPATA TAARIFA KATIKA MFUMO WA UTOAJI TAARIFA ZA TARATIBU ZA BIASHARA ZA KIMATAIFA

Mfumo wa utoaji taarifa za taratibu za biashara za Kimataifa unatoa taarifa za taratibu za kupata leseni, vibali na taratibu za kiforodha kwa bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi, zinazoingizwa nchini na zinazopitishwa kwenda nchi nyingine.

Mfumo wa utoaji taarifa za taratibu za biashara za Kimataifa unatoa taarifa hatua kwa hatua katika mchakato wa kuomba vibali au leseni. Kila hatua inaonyesha wapi uende, unamuona nani, nyaraka zipi unazopaswa kwenda nazo, fomu unazotakiwa kujaza, gharama utakazolipa, sheria inayokuongoza katika hatua husika na mahali pa kulalamika endapo hujaridhika na huduma au kupata tatizo. Taratibu zimewekwa kwa mtazamo wa upande wa mteja na sio kwa mtazamo wa upande wa taasisi. Kila mteja anapoonana na mtoa huduma inahesabika kuwa ni hatua.

Namna ya kupata taarifa katika Mfumo wa utoaji taarifa za taratibu za biashara za Kimataifa

- 1) Tembelea tovuti Mfumo wa utoaji taarifa za taratibu za biashara za kimataifa <https://business.go.tz/> au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz kisha bofya **Trade Information Module**.
- 2) Kupitia <https://business.go.tz/> nenda kwenye **"How Do I"** kisha bofya **"Import & Export"**
- 3) Soma maelezo ya mwanzo kuhusu mfumo
- 4) Kisha tumia 'kisanduku' cha kuchagua bidhaa unayoitaka. Chagua aina ya huduma **"Type of operation"** (Export or Import or Transit) kisha chagua aina ya budhaa **"Type of commodity"** (kuna bidhaa tofauti tofauti unaweza chagua yoyote kulingana na uhitaji wako), Kisha bofya palipoandikwa **"Search"**
- 5) Utapata taarifa mbalimbali kuanzia taratibu za awali **"Preliminary registration and**

licences",Vibali "Permit", na Taratibu za Kiforodha **"clearance"** na taarifa za ujumla kwa mteja wa mara ya kwanza **"full procedure for the first time trader"**.

- 6) Bofya katika sentensi zilizopigiwa mistari yenye nukta ili kuweza kupata taarifa kuhusu bidhaa uliyoichagua (Maneno yaliyopigiwa mistari ni majina ya taratibu ambazo mfanyabiashara anapaswa kufuata ili aweze kupata kibali au leseni na taratibu za kiforodha.
- 7) Kwenye baadhi ya taratibu kuna vitufe vya kuchagua aina ya kibali au lango la kutolea/kuingizia bidhaa utaona **"select an option"** au **"Select exit/entry point"** . Bofya kisanduku cha kuchagua ili kuweza kupata taarifa za taratibu unazozitaka.
- 8) Baadhi ya hatua zinatoa huduma kwa njia ya mtandao hivyo kupata huduma hizo bofya kisanduku kilichoandikwa **"Apply online"** au **"Obtain online"**

HUDUMA KWA WATEJA:

0735 331 001, 0735 000003, 0735 331 004

P. O. Box 9393, Dar es Salaam - Tanzania
Tel: +255 22 218 0139, 218 1344,
218 0113, 2180141, Fax: +255 22 218 0371
Email: usajili@brela.go.tz, ceo@brela.go.tz,
Web: www.brela.go.tz



HATUA KWA HATUA YA JINSI YA KUOMBA
TAARIFA RASMI ZA KAMPUNI NA
MAJINA YA BIASHARA KWA
NJIA YA MTANDAO, MFUMO WA
KIELEKTRONIKI WA UTOAJI WA LESENI
ZA BIASHARA NA ZIJUE HATUA ZA
KUPATA TAARIFA KATIKA MFUMO
WA UTOAJI TAARIFA ZA TARATIBU
ZA BIASHARA ZA KIMATAIFA

HATUA KWA HATUA YA JINSI YA KUOMBA TAARIFA RASMI ZA KAMPUNI NA MAJINA YA BIASHARA KWA NJIA YA MTANDAO

1. Tengeneza Akaunti ya ORS
 2. Ingia kwenye: "E services for Registered Users"
 3. Bofya "New E Service"
 4. Bofya: "Information Services"
 5. Bofya "Request for standard search result" au "Request for custom search result"
 6. Baada ya kusoma maelezo na kuchagua chaguo sahihi; bofya "Proceed"
- a) Kama umechagua "Request for a standard search result," unatakiwa kufanya yafuatayo baada ya kubonyeza "Proceed:"
1. Ingiza namba ya kampuni/jina la biashara husika kisha bofya "Search." Baada ya kusoma na kuchagua unachotaka kujibiwa bonyeza Proceed
 2. Baada ya kuingiza "Represantaion Statement" bofya "Proceed" kutengeneza malipo/Payment
 3. Baada ya kulipia, pakua risiti kisha subiri majibu.

NB: Majibu ya "Standard searches" hutokea yenyewe papo kwa papo

- b) Kama umechagua "Request for a custom search result," unatakiwa kuchagua yafuatayo:
1. Chagua "Tailor Made", kisha bofya "Proceed"
 2. Ingiza namba ya kampuni/Jina la Biashara kisha bofya "Search", ambapo jina la Kampuni/Jina la biashara utafutaji wako litatokea kisha ingiza "Description of the search" kisha chagua "Delivery Mode" kisha bofya Proceed.

3. Jaza "Represantaion Statement" kisha bofya "Proceed" kutengeneza malipo/Payment
4. Baada ya kulipia, pakua risiti kisha subiri majibu

NAMNA YA KUFUATILIA MAENDELEO YA MAOMBI YAKO

Angalia upande wa kushoto ndani ya mfumo , bonyeza sehemu ya Maombi(Applications)

Tazama sehemu ya "Imefanyiwa kazi?" Kama ni "Yes" inamaanisha ombi lako limeshughulikiwa hivyo bofya "View" kuangalia taarifa zaidi ikiwemo kupakua barua yako.

Kama "Imefanyiwa kazi?" insemu "NO" na sehemu ya Under "Hatua ya kazi":-

- Inasema "Process and Enter Recommendation" inamaanisha maombi yako BRELA na yanafanyiwa kazi.

MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UTOAJI WA LESENI ZA BIASHARA

Ili uweze kutumia mfumo huu kwa ajili ya maombi ya leseni za Biashara inakubidi uwe umejisajili katika mfumo.

Kujisajili katika mfumo huu unatakiwa kuwa na vifuatavyo:-

- a. Anwani hai ya Barua pepe ya Kampuni au Biashara husika;
- b. Namba ya simu inayopatikana wakati wote.

Ili kujisajili tembelea katika tovuti www.business.go.tz kisha bonyeza kitufe cha Jisajili na kufuata maelekezo.

MASHARTI YA MUHIMU KWA MAOMBI YA LESENI ZA BIASHARA

1. Mtu Binafsi

- a. Kitambulisho cha mwombaji wa Leseni, kama Kitambulisho cha Taifa, Hati ya kusafiria (Pasipoti), Kitambulisho cha mpiga kura au

- cheti cha kuzaliwa (kwa raia wa Tanzania);
- b. Hati ya Mlipa kodi (TIN Number ya Biashara);
- c. Uthibitisho wa kuwa ana mahali pa Kufanya biashara (Mfano. Mkataba wa pango wa Ofisi, Leseni ya Makazi au Hati ya Ardhi)
- d. Uthibitisho wa kutokudaiwa kodi (Tax Clearance Certificate); na
- e. Kibali kutoka kwenye mamlaka za udhibiti (Wizara, Mamlaka, Idara, Taasisi au Wakala za Serikali) kwa biashara zinazodhibitiwa na Mamlaka za Serikali.

2. Kampuni na Majina ya Biashara

- a. Hati ya Usajili wa Kampuni (Certificate of Incorporation) au Jina la Biashara (Certificate of Registration and Extract),
- b. Mkataba wa Makubaliano kati ya Wabia (Partnership deed) au Memorandum and Articles of Association.
- c. Hati ya Mlipa kodi (TIN Number);
- d. Uthibitisho wa kutodaiwa kodi (Tax Clearance Certificate) kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA)
- e. Mkataba wa pango uliothibitishwa na Mwanasheria na kulipiwa kodi (Lease Agreement with Advocate stamp and stamp duty fees paid);
- f. Uthibitisho wa uraia kwa wenye hisa (Proof of shareholder's citizenship) kama Hati ya kusafiria (Pasipoti), Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha kupigia kura au cheti cha kuzaliwa (kwa raia wa Tanzania); au Kibali cha kuishi nchini daraja ya "A" kwa wenye hisa wasio Watanzania na Daraja ya "B" kwa wakurugenzi wa kampuni au biashara wasio watanzania; na
- g. Kibali kutoka kwenye mamlaka ya udhibiti (Wizara, Mamlaka, Idara, Taasisi au Wakala za Serikali) kwa biashara zinazodhibitiwa na Mamlaka za Serikali.